

## Nyimbo kama Mkakati wa Kuimarisha Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika: Uchunguzi wa Nyimbo za Kampeni za Wachuka

*Onesmus Gitonga Ntiba<sup>1</sup> na Kineene wa Mutiso<sup>2</sup>*

<sup>1</sup>*Chuo Kikuu cha Mount Kenya, Kenya*

<sup>2</sup>*Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya*

### Ikisiri

Katika makala haya, tumeangazia namna nyimbo za kampeni zinaweza kutumika kuimarisha mshikamano wa kitaifa na uwiano Barani Afrika. Nyimbo za kampeni tunazotilia maanani katika mjadala huu ni zile zilizokuwa zikiimbwa toka 1992-2013 katika jamii ya Wachuka. Makala haya yanatambua ukweli kwamba wanasiasa hutumia si nyimbo tu bali hutumia hotuba, maandishi na hata pesa kuweza kuyapata mamlaka ya kisiasa na hata kujidumisha hapo baada ya kuyapata. Katika mjadala huu, tunaongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (U.U.H). Tutaelezea Wachuka ni kina nani na wanapatikana wapi. Katika uchanganuzi wetu, tutaangalia muktadha wa nyimbo hizi, wahusika wanaopatikana mle, ujumbe uliomo na jinsi lugha ya ushawishi inavyotumika kuuwasilisha. Katika lugha, tutajikita katika masuala matatu: vipashio vya lugha, mshikamano na mtindo unaotumika kuuwasilisha ujumbe wa ushawishi. Baada ya kuyashughulikia masuala hayo yote, tutahitimisha makala yetu kwa tumaini kuwa tutakuwa tumedhihirisha jinsi nyimbo zinaweza kutumika kuleta muumano wa kitaifa na uwiano Barani Afrika kwa manufaa ya wote.

**Maneno Muhimu:** Nyimbo za Kampeni, Wanasiasa, Usemi, Ushawishi.

### Utangulizi

Fasihi ni sanaa ambayo inahusisha ubunifu kwa kiasi kikubwa. Ubunifu huu hasa katika nyimbo una uwezo wa kuibua hisia na kuathiri mitazamo ya wanaozisikiliza. Katika muktadha wa makala haya, nyimbo za kampeni ni nyimbo za kisiasa zinazolenga kuwashawishi wapiga kura. Ngure (2003) na Matei (2011) wanahoji kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, ni shughuli chache sana zisizoambatana na nyimbo, densi na ngoma. Nyimbo huwa na ujumbe

unaowasilishwa kwa mitindo ya kipekee inayoambatana na shughuli zinazotekelezwa.

Kwa mujibu wa Nyairo na Ogude (2005), nyimbo za kisasa zina historia ndefu nchini Kenya na barani Afrika. Zimetumika kabla na baaada ya uhuru kuyatekeleza majukumu mbalimbali. Wakati wa ukoloni, zilitumika kwa kukuza na kuendeleza ujitambuaji wa kijamii pamoja na kuwahamasisha wanajamii kuweza kuchukua na kugomea udhalimu wa wakoloni. Baada ya uhuru nyimbo hizi zimetumika kudumisha uzalendo wa kitaifa. Pia zimetumika kushawishi watu kisiasa kuandama na kufuata sera fulani za kisiasa. Nchini Kenya, wakati wa uchaguzi mkuu au mdogo, nyimbo hizi hutumika pakubwa kwa lengo la kuwafanya wapiga kula kuwapigia wanasiasa fulani kura zao. Kama ilivyo katika jamii nyingi nchini Kenya na barani Afrika, nyimbo hizi zimetumika kwa njia hasi au chanya. Waandishi wa makala haya wanatambua ukweli kuwa zikitumiwa kwa njia chanya, zinaweza kuchangia uimarishaji wa mshikamano wa kitaifa na uwiano barani Afrika.

### **Nadharia**

Makala haya yataongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (U.U.H). Chimbuko la nadharia hii ni mawazo ya Fowler, Kress na Hodge (1979) kuhusu Isimu Hakiki. Fairclough (2001) anasema kuwa umilisi wa lugha huwawezesha baadhi ya watu katika jamii kupata nguvu zinazowawezesha kuwatawala wengine. Katika makala haya, tunauchukulia wimbo kama usemi unaoweza kuchanganuliwa. Kwa mujibu wa Wodak (2001), nadharia hii ina mikondo mitatu ya kiutumikizi:

**Mkondo I** : Mkondo unaochukulia usemi kama matini inayojitosheleza.

**Mkondo II:** Mkondo unaosisitiza ujumbe/maudhui iliyomo katika usemi husika.

**Mkondo III:** Mkondo unaochangamkia ufasiri wa kinachowasilishwa katika usemi husika.

Tutazingatia mikondo hii mitatu kuangazia jinsi nyimbo za kampeni zinaweza kutumiwa kuimarisha mshikamano wa kitaifa na uwiano Barani Afrika.

### **Jamii ya Wachuka**

Jamii ya Wachuka ni mojawapo wa makundi saba ya Wameru wanaozungumza lahaja mbalimbali. Wachuka huizungumza lahaja ya Kichuka. Lahaja hizo zingine za Kimeru ni Kitharaka, Kimuthambi, Kimwimbi, Kiimenti, Kitigania na Kiigembe. Mukuthuria (1997) anakiri kuwa kujumuisha Kitharaka na Kichuka katika kundi la lahaja za Kimeru kumezua mjadala mkali miongoni mwa wasomi. Kwa mfano, Wa Mberia (1993) anadai kuwa Kitharaka na Kichuka ni lugha na si lahaja za Kimeru.

Guthrie (1967) anadai kuwa Wachuka ni miongoni mwa makundi ya Wameru wanaosemekana kuwa walitoka katika kisiwa cha Mboa kilicho katika mwambao wa Afrika mashariki kwa sababu ya unyanyasaji na watawala wanaorejelewa kama ‘Nguo Ntune’ (Nguo Nyekundu). Inaaminika kuwa hawa walikuwa Waarabu waliokuwa wakifanya biashara katika janibu hizo. Kulingana na Mwaniki (1982), tamaduni simulizi za Wachuka na Watharaka zadai kuwa jamii ya Wachuka ina uhusiano wa karibu zaidi na jamii ya Watharaka. Kwa mujibu wa simulizi hii, Chabugi alikuwa na wake wawili: Ciambandi na Ciangoi. Ciambandi ndiye alikuwa mkewe wa kwanza wa Chabugi. Watoto aliopata naye ndio mababu wa Watharaka. Wale aliopata na mke wa pili, yaani Ciangoi nao ndio mababu wa Wachuka. Mtafaruku wa kifamilia ulitokea na Ciangoi na wanawe wakatorokea maeneo karibu na msitu wa Mlima Kenya. Ciambandi na watoto wake waliachwa nyikani mahali panapoitwa Maria Nkanga.

Were na Wilson (1972) wamesema kuwa Wachuka ni mojawapo ya makundi ya Wabantu wanaopatikana karibu na Mlima Kenya. Walifika katika maeneo waliko sasa katika Karne ya Kumi na Tatu B. K. Kwa upande wa Kaskazini, wanapakana na msitu wa mlima Kenya, upande wa Mashariki wanapakana na Wamuthambi na Wamwimbi, upande wa Kusini wanapakana na Watharaka na Wambeere na kwa upande wa Magharibi wanapakana na Waambu. Hivi leo, lahaja ya Kichuka inazungumzwa katika wilaya ya Meru Kusini katika tarafa za Chuka, Magumoni na Igambang’ombe. Maeneo haya yote hupatikana katika kaunti ya Tharaka Nithi, Kenya. Zamani, kiuchumi Wachuka walijishughulisha na ukulima na ufugaji wa wanyama kama vile ng’ombe, mbuzi na kondoo. Baada ya maingilio ya wakoloni, na hasa dini ya Kikristo, utamaduni wa jamii hii ulianza kupata athari za kimagharibi. Asasi za kitamaduni na vikorombwezo vya kitamaduni viliporomoka. Wakati itikadi ya kuwachagua viongozi wa kisiasa ilianza na kukita mizizi nchini Kenya, Wachuka kama ilivyokuwa katika jamii zingine nchini Kenya walianza kuimba nyimbo za kampeni. Kwa sasa, nyimbo hizi huchukua nafasi kubwa sana wakati kuna uchaguzi mkuu au mdogo.

### **Muktadha wa Nyimbo za Kampeni za Jamii ya Wachuka**

Utungo wowote ule huwa katika muktadha fulani. Msanjila (1989) na Mathooko (2007) wanasema kuwa suala la muktadha ni muhimu sana hasa katika isimujamii. Wanachukulia muktadha kama kipengele muhimu cha isimu hasa wakati mchanganuzi anataka kupata welewa wa kina wa usemi fulani. Umuhimu wa kuangalia nafasi ya muktadha katika makala haya umekitwa katika ukweli kuwa kila jambo au tukio hufanyika katika mahali fulani. Msokile (1993) anasema kuwa kila utungo una makulia yake. Mtunzi hatungi katika ombwe tupu bali hujikita katika muktadha fulani maalum wa kijiografia, wakati maalum wa kihistoria au jamii yenye sifa fulani. Nyimbo za kampeni za Kichuka ambazo tumetambalia katika makala haya ni aina ya usemi uliomuktadhalishwa; yaani ni usemi uliowekwa katika mahali na wakati maalum. Nyimbo za kampeni za

Kichuka zinachota malighafi na masuala yanayoshughulikiwa kutokana na jamii yenyewe. Katika makala haya, tunagusia muktadha wa kimahali, kiwakati na kitamaduni. Kwanza, tutaangazia muktadha wa kimahali. Tuliweza kutambua aina tatu za muktadha wa kimahali:

- a) Mahali maalum kijiografia.
- b) Mahali pa kawaida.
- c) Urejelezi wa mahali kijazanda.

Katika urejelezi wa mahali kijiografia, kuna kuyataja mahali katika kaunti ya Tharaka Nithi na hata nje ya nchi ya Kenya. Mathalani kuna kutaja maeneo kama vile Chuka, Nithi, Chuka Igambang'ombe, Muthambi, Tharaka, Mwimbi, Jerusalem na Hague. Mfano katika muktadha wa nyimbo:

**Kif.**

*Antu ma Chuka Igambang'ombe,  
Kura ni kwa Muthomi,  
Tutikwenda mangi,  
Kura cietu ni ciake.*

**Kif**

*Ni sinita wa ngubu,  
Na ni wakili munene,  
Agendaga nkinya Hague.  
Kumatetera Akenya,  
Ni Kindiki ni Kindiki,  
Uria ukuga tiwe niwe.*

**Tafsiri**

Wakaaji wa Chuka Igambang'ombe,  
Kura ni kwa Muthomi,  
Hatutaki wengine,  
Kura zetu ni zake.

**Tafsiri**

Ni seneta wa nguvu,  
Na ni wakili mkubwa,  
Yeye huenda hata Hague.  
Kuwatetea Wakenya,  
Ni Kindiki ni Kindiki,  
Asemaye siye ajue ndiye.

Urejelezi wa mahali pa kawaida ni kama pale nyimbo zinataja bunge na baraza. Haya ni mahali ambapo wanaochaguliwa katika nyadhifa mbalimbali huenda kuwashughulikia waliowachagua. Urejelezi wa mahali kijazanda ni kama pale wimbo unarejelea eneo bunge la Chuka Igambang'ombe kama boma (mucii) au 'shamba la nyani.' Angalia urejelezi huu katika muktadha wa vifungu vya nyimbo za kampeni za Kichuka:

**Kif.**

*Ndungamirira:  
Nkinye mucii uyu  
Giria ukinywa mbere:  
Ni ntuuri ii*

**Kif**

*Mugunda wa maguna:  
Karabacha!*

**Tafsiri**

Nisimamie:  
Niingie boma hili  
Kabla halijaingwa:  
Ni jinga hili.

**Tafsiri**

Shamba la nyani:  
Karabacha!

*Iiruri:*

*Karabacha*

Iiruri:

Karabacha

Urejeleaji wa mahali una maana chungu nzima. Kwanza, kupitia kwake, wanasiasa wanajenga nguzo muhimu kuwa wao ni kitu kimoja na kwa sababu hiyo wanafaa kushirikiana kuwachagua viongozi fulani. Akizungumzia juu ya urejeleaji kimahali, Senkoro (1987) anasema kuwa wahusika katika matini lengwa huonekana wakiwa na mahali pa kuwashikilia. Pili, urejeleaji huu unaleta ushabahi kweli.

Baada ya kushughulikia muktadha wa kimahali, hebu sasa tuangazie muktadha wa kiwakati. Nyimbo za kampeni za Kichuka zinaweza kuwekwa katika muktadha fulani wa kiwakati. Majina ya wanasiasa katika nyimbo hizi yanaweza kuhusishwa na kipindi fulani cha kihistoria katika mapisi ya Wachuka. Majina haya ya wanasiasa ni kama vile Njoka, Kapteni, Petkay, Kareke, Nthuraku Gichuyia, Kaburu, Muthomi Njuki, Mbaabu, Mati, Njeru na Karagita. Wale wengi wamerejelewa kwa sehemu moja ya jina ili kuweza kuyahifadhi mapigo ya kimziki katika nyimbo hizo. Mwaka wa 1991 kifungu cha pili (A) cha katiba ya Kenya kilibadilishwa kuruhusu vyama vingi vya kisiasa nchini Kenya. Jambo hili lilizua msisimko wa kisiasa katika maeneo mengi nchini Kenya; Nithi ikiwepo. Waliokuwa wakichukia chama cha KANU na uongozi wake walipata nafasi ya kuimwaga dukuduku yao kuzipitia nyimbo za kampeni katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 1992.

Angalia:

**Indi ninkinyu**

**Kif 1-2**

*Indi ninkinyu:*

*Nithi yonthe iii*

*Ya kubadilisha:*

*Nguku ninkwiu ii*

**Tafsiri**

Sasa ndo wakati:

Nithi nzima.

Ya kubadilisha:

Kuku amekufa.

*iii wa kathimbu:*

*Tutikumwenda iii*

*Indi ninkinyu:*

*Ya kubadilisha ii*

Huyu mwenye rungu:

Hatumtaki

Sasa ndo wakati:

Wa kubadilisha.

Kuku ni jazanda inayosimamia chama cha kisiasa cha KANU. Waimbaji katika wimbo huu wanasema kuwa ‘kuku amekufa; yaani chama cha KANU kimepoteza umaarufu. Kabla ya kuyagawanya katika maeneo bunge mawili mwaka wa 2012, eneo bunge la Nithi lilijumlisha Chuka Igambang’ombe na Maara. Kwa hivyo, mzozo wa kimaeneo kati ya Wachuka, Wamuthambi na

Wamwimbi ulidhihirika katika nyimbo hizi za kampeni. Hii ndiyo sababu waimbaji wa Chuka katika wimbo ‘*mbumbui*’ (buibui) wanasema Kareke (anayetoka Mwimbi) aumizwe buibui. Kuumizwa buibui ni kukosa kupewa kura. Kwa mfano:

**Kichuka**

Na Kareke:

*Niarumithue mbumbui*

*Ya matina:*

*Agendage nayo.*

**Tafsiri**

Na Kareke:

Aumizwe buibui

Ya matakoto:

Awe yuande naye.

Katika uchunguzi wa nyimbo za kampeni za Kichuka, uchunguzi wa muktadha wa kiwakati ni muhimu kama ilivyo ule wa kimahali. Katika nyimbo za kampeni waimbaji wanarejelea matendo ya wakati uliopita kama sababu ya kuchukua hatua muhimu kwa sasa kwa kuwachagua wanaofaa kwa maisha mema sasa na baadaye katika eneo hili la Chuka. Utamaduni unahusu jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Kwa hivyo, muktadha wa kitamaduni unahusu amali na desturi za jamii za kila siku. Wodak (1995) anatoa mawazo ya kijumla kwamba suala la muktadha wa kitamaduni wa usemi wowote ule unaochunguza ni kigezo muhimu cha kutilia maanani kama usemi huo utaweza kufasirika kikweli. Katika nyimbo za kampeni za Kichuka, waimbaji wanaonyesha welewa wa utamaduni wa mila na matukio ya kijamii ya Wachuka. Nyimbo hizi huwa zina cheche fulani za itikadi na desturi za jamii ya Wachuka. Katika nyiso za Wachuka, kuna wimbo maarufu unaitwa ‘*Nthaka ni kithaka*’ (Ghulamu ni kichaka). Katika kipindi cha kisiasa tulichoangazia, wimbo huu ulifaraguliwa na kuwa wa kisiasa. Kwa mfano:

**Kichuka**

*Nthaka, nthaka, nthaka,*  
*Nthaka ni kithaka nthaka:*  
*Igendaga mbere ya riua,*  
*Nthaka:*  
*Igendaga na rukororima:*

**Tafsiri**

Ghulamu, ghulamu, ghulamu,  
Ghulamu ni kichaka ghulamu:  
Hurauka kabla ya jua kuchomoza  
Ghulamu:  
Hurauka asubuhi sana.

Katika wimbo huu, waimbaji wanasema kuwa vijana wa mwanasiasa fulani huamka asubuhi sana kwenda kumpigia kura. Katika jamii ya Wachuka, kuna miiko na mikatazo ya kutumia lugha kwa uwazi, hasa kuhusiana na matusi au karaha ya aina fulani. Kwa sababu hii, imejiwekea shuruti kutotumia maneno fulani waziwazi. Hata hivyo, katika nyiso za Wachuka, makatazo ya aina hii hayafuatiliwi katika msimu wa tohara. Wimbo huu wa kisiasa umetumia maneno ya karaha kwa sababu ni wimbo wa tohara ambao umefaraguliwa. Umetaja sehemu za siri, jambo ambalo ni muhali kufanya katika jamii ya Wachuka katika hali ya kawaida. Mathalani:

**Mugunda wa maguna**

**Vif. 2-3**

Giki ni kithii:

*Karabacha!*

*Iiiruri:*

*Karabacha!*

Gia kuthia mbene:

*Karabacha!*

*Iiiruri:*

*Karabacha!*

**Shamba la Wanyama**

**Tafsiri**

Hiki ni kinu:

*Karabacha!*

*Iiiruri:*

*Karabacha!*

Ni cha kusaga kuma:

*Karabacha!*

*Iiiruri:*

*Karabacha!*

**Wahusika katika Nyimbo za Kampeni za Kichuka**

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika usemi wowote. Madumulla (2009) anasema kuwa ni kupitia wahusika msanii huwasilisha ujumbe wake. Baadhi ya wahusika wanaopatikana katika nyimbo za kampeni za Kichuka ni wa kihalisia hata kama kuna wakati waimbaji wanawabuniliza. Wahusika hawa ni nyenzo kuu katika nyimbo hizi. Sababu ni kuwa wao ndio jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika wimbo husika. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa mgogoro wa kisiasa unaotandarukiwa katika nyimbo hizi za kampeni za Kichuka unazungukia wahusika hawa. Ujumbe unaoendelezwa katika nyimbo hizi za kampeni hauwezi kudhihirika pasipokuwa na mhusika au wahusika ambao wanapitisha ujumbe huo kwa walengwa fulani. Katika makala haya, tumeweza kuwatambua wahusika wa aina nne:

**Wahusika Wanasisia Halisia**

Hawa ni wanasisia waliokuwa wakigombea nyadhifa mbalimbali za kisiasa. Katika nyimbo za kampeni za Kichuka tulizopata katika data tuliyokusanya, tuliweza kuwatambua wahusika wanasisia halisia 15. Hii haimanishi kuwa hakukuwa na wengine. Hawa ni wale majina yao yalitajwa moja kwa moja katika nyimbo za kampeni tulizoimbiwa. Hawa ni wahusika wa kikweli katika muktadha wa kisiasa katika kipindi kati ya 1992-2013 katika tarekhe ya jamii ya Wachuka. Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya wahusika hawa:

<b>Mwanasisia</b>	<b>wadhifa aliokuwa akipigania</b>	<b>kipindi</b>
Njoka Mutani	ubunge	1992, 1997
Kapteni	ubunge	1997, 2002
Petkay Miriti	ubunge, ugavana	2002, 2007, 2013
Muthomi Njuki	ubunge	2013
Beatrice Nkatha	ubunge	2013

Kindiki

useneta

2013

Tumetanguliza kwa kudokeza kuwa wahusika wanasiasa halisia ndio walikuwa katikati ya mchakato wa kuomba mamlaka ya kisiasa katika eneo hili. Makala haya yanatambua kuwa kulikuwa na urejelezi wa majina yao na wadhifa waliokuwa wakitaka katika nyimbo za kampeni za Kichuka. Baada ya kuwatambua kwa majina yao, waimbaji walipiga hatua kwa kuangazia uzuri au ubaya wao ili angalau wapewe kura au wanyimwe.

### **Wahusika Wanasiasa Zungumza**

Wahusika wanasiasa zungumza ni wale waimbaji wa nyimbo za kampeni za Kichuka. Hawa wahusika hawatambuliwi kwa majina maalum kama ilivyo katika wahusika wanasiasa halisia. Katika nyimbo hizi, wanatambuliwa kwa kiwakilishi nafsi 'tu' katika wingi.

#### **K.m.**

##### **Kif.**

*Na Gichuiyia:*

*Tharathara maguru*

*Tukubire:*

*Na mbunge ii*

##### **Tafsiri**

Gichuiyia:

Harakisha miguu

Tukupeleke:

Bunge.

Hawa wahusika ndio wanaimba, wanabembeleza, wanakashifu, wanaomba kwa niaba ya na kadhalika. Kila wakati na katika uimbaji wao, wangetaka kujidhihirisha kama watu wanaojua jamii ya Wachuka inataka nini na ni nani anafaa kuchaguliwa. Wanapoimba, wanajirejelea kwa namna ya kuonyesha wao ni wengi mno. Hii ni njia tu ya kupalilia kura kwa mwanasiasa halisia wanayepigia debe.

### **Wahusika Ombwa**

Wahusika ombwa ndio walengwa wa ujumbe katika nyimbo za kampeni za Wachuka. Hawa ni wahusika muhimu sana kwa sababu ndio wapiga kura. Kura waliyo nayo ndiyo inawafanya wahusika wanasiasa halisia na zungumza wawarai, wawabembeleze, wawatukuze na kuwahimiza angalau waweze kuwapigia kura wanasiasa wanaoomba zile kura. Wahusika wanasiasa zungumza wanawaonyesha manufaa watakayopata kwa kumchagua yule wanayepigia debe.

### **Wahusika Rejelewa Kifiche**

Hawa ni wahusika ambao wanalengwa na wahusika wanasiasa zungumza kwa mbali. Hawataki kujitokeza kimasomaso kuwa wanawasema kwa ubaya kuuepuka mgogoro wazi katika kinyang'anyiro hiki cha kuzisaka kura kutoka kwa wahusika ombwa. Japo wanawalenga kwa mbali, kwa wenyeji wa eneo husika wanajulikana. Kwa mfano:

##### **Kichuka**

*iii wa kathimbu*

##### **Tafsiri**

Huyu mwenye rungu.



*Tutikumwenda ii*

Hatumtaki.

Mhusika fiche anayerejelewa kwa maneno ‘wa kathimbu’ (huyu mwenye rungu) ni Rais mstaafu Daniel arap Moi. Katika uchaguzi wa 2013, tunazipata nyimbo kadhaa zilizokuwa zinarejelea wapinzani wa baadhi ya wanasiasa kwa njia ya ufiche. Katika wimbo unaoitwa ‘*tumuthureni*’ (tumchagueni) waimbaji wanawahimiza wapiga kura wampigie Muthomi Njuki kura ili aweze kuwa mbunge wa eneo bunge la Chuka Igambang’ombe. Wanawaomba wapiga kura wasithubutu kuchagua ‘*garagara*’ (watu wasio na maana). Hawa wanasiasa wengine wasio na maana hawatajwi. Angalia:

**Kichuka**

***Tumuthureni***

*Antu ma Chuka Igambang’ombe*  
*Kura ni kwa Muthomi,*  
*Tutikwenda mangi,*  
*Kura cietu ni ciake.*  
*Tigana na garagara.*  
*Kura cietu ni ciake,*  
*Tuthure maendeleo,*  
*Nitumuthureni,*  
*Nikenda tuthii na mbere.*

**Tafsiri**

**Tumchagueni**

Wakaaji wa Chuka Igambang’ombe  
Kura ni kwa Muthomi,  
Hatutaki wengine,  
Kura zetu ni zake.  
Acha watu wasio na maana  
Kura zetu ni zake,  
Tuchague maendeleo,  
Tumchagueni,  
Ili tuweze kwenda mbele.

Wahusika tuliowashughulikia katika sehemu hii si kama wale tunaowapata katika kazi za kibunilizi kama riwaya na tamthilia. Hawa ni wahusika wanaopatikana katika matukio halisi katika tarekhe ya jamii ya Wachuka. Pia tunaweza kusema kuwa ni wahusika wanaopatikana katika mgogoro wa kikweli wa kisiasa katika jamii lengwa nchini Kenya.

**Ujumbe katika Nyimbo za Kampeni za Kichuka**

Uimbaji wa nyimbo za kampeni na wanasiasa wa jamii ya Wachuka huwa na lengo la kupitisha ujumbe fulani kwa walengwa wa huo wimbo. Ujumbe huu ndio unatarajiwa kuwafanya wapiga kura wawapigie wanasiasa fulani kura zao. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa ujumbe ni taarifa au habari inayopatikana katika matini fulani. Katika muktadha huu, ni taarifa au habari inayopatikana katika wimbo wa kampeni. Habari au taarifa hutolewa na mwasilishi na huwa inalenga hadhira au wapokezi fulani. Kwa hivyo, katika nyimbo za kampeni za Kichuka, wahusika wanasiasa zungumza ndio wanatoa taarifa au habari ambazo zinawalenga wapiga kura. Ujumbe katika nyimbo hizi za kampeni za Kichuka ulichukua mikondo miwili. Mkondo wa kwanza ni pale ujumbe katika wimbo lengwa ni wa kumjenga kwa kumsifu mwanasiasa fulani kutoka mwanzo hadi mwisho. Mkondo wa pili ni pale ambapo katika wimbo husika, kuna mwanasiasa anayesifiwa na wakati huo huo kuna mwanasiasa anayekashifiwa. Mbali na kusifu na kukashifu, kuna nyimbo ambazo zina ujumbe

wa maendeleo ambapo mwanasiasa fulani amelenga kuyaleta katika eneo fulani la uwakilishi. Katika nyimbo hizi, tunapata ujumbe wa umaeneo, maudhi na mabadiliko ya kisiasa. Katika kuwasilisha ujumbe wao katika nyimbo hizi, wanasiasa wanatumia mitindo ambayo inawasaidia kujijenga na wakati huo huo kuwabomoa wapinzani wao.

### Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Kampeni za Jamii ya Wachuka

Katika matumizi ya lugha, tutaangazia mambo matatu:

- Vipashio vinne vya lugha: sauti, silabi, maneno na vifungu vya maneno.
- Mtindo.
- Mshikamano.

Lahaja ya Kichuka ina jumla ya sauti saba za vokali. Hizi ni {a}, {ε}, {i} {⊃}, {u}, {ĩ}, {ũ}. Kati ya hizi saba, nne ndizo zinatumiwa kujenga mshikamano katika nyimbo husika. Sauti hizi ni {a}, {i}, {ĩ} na {ũ}. Sauti hizi zinasaidia kuleta mshikamano na hata kujenga wizani au ridhimu, kwa mfano:

#### Kichuka

#### Tafsiri

*iiiiaaiiui kiatho kiria gigukinya:*

iiiiaaiiui ile siku imefika:

*iiiiaaiiui kiatho kiria gigukinya*

iiiiaaiiui ile siku imefika

Silabi nyingi katika lahaja ya Kichuka zina mapendeleo ya mpangilio wa silabi wa *KVKV* (Konsonanti, vokali, konsonanti, vokali) katika kule kujenga maneno yake. Mkondo huu uliwezesha waimbaji kuyatohoa baadhi ya maneno ya Kiingereza ili yaweze kutumika katika nyimbo za kampeni katika jamii hii. Mathalani:

#### Kiingereza

#### Tafsiri(Utohozi)

*County*

Kaunti

*Governor*

Ngabana

*Senator*

Sinita

*County representative*

Kaunti rebu

*Mister*

Mista

*Parliament*

Baliamenti

Kwa mujibu wa Yule (1985), maneno ni vipengele vya lugha ambavyo ni vidogo na huru. Kila kipengele cha neno huweza kutamkika peke yake. Msingi wa lugha inayopatikana katika nyimbo za kampeni za Kichuka ni maneno yanayotumiwa mle na wanasiasa. Maneno haya ni rasilmali ya kimsingi ambayo wanasiasa hutumia kuwasilisha ujumbe wao. Njogu (2001) anasema kuwa wanasiasa wanaohusika hutumia rasilmali hiyo ya maneno kujenga ulimwengu wa nyimbo zao na kuyawasilisha masuala tofauti yanayoibuka katika eneo lao. Katika nyimbo hizi kuna matumizi ya maneno unde kama vile ‘*murembeko*’ katika wimbo unaitwa ‘*mrembo*’ (*murembo*). Neno hili limetokana na neno

‘murembo.’ Katika muktadha wa nyimbo hizi neno hilo limeundwa na waimbaji kuleta kinyume cha ‘mrembo’ yaani ‘sura mbaya.’ Linatumika hivi katika wimbo:

**Kichuka**

*Muthomi ni:*

Murembo:

*Mau mangi ni:*

Murembeko.

**Tafsiri**

Muthomi ni:

Mrembo:

Hao wengine ni:

Sura mbaya.

Katika nyimbo hizi za kampeni za jamii ya Wachuka, nomino za pekee, vitenzi na vivumishi vimetumika kwa lengo maalum. Nomino za pekee zinazotumika kwa wingi ni majina ya wanasiasa na maeneo wanayotoka. Baada ya kuwadhihirisha wanasiasa lengwa na maeneo wanayotoka, wanatumia vitenzi kuonyesha matendo yao. Wanaonyesha mambo ambayo wanasiasa lengwa washafanya, wanayofanya au wanayonua kufanya wakipewa mamlaka ya kisiasa. Aina ya vivumishi vinavyotumika katika nyimbo hizi ni vivumishi vya sifa, vivumishi viashiria na vivumishi vimilikishi. Vivumishi vya sifa vinavyotumika vinaonyesha wanasiasa wanaoomba kura ni watu wa aina gani. Vivumishi viashiria navyo vimetumika kuwaashiria hawa wanasiasa na maeneo wanayotoka. Vivumishi vimilikishi vimetumika pale ambapo wahusika wanasiasa wazungumza wangetaka kuonyesha uhusiano wa karibu walio nao na mwanasiasa anayetaka kupewa wadhifa fulani. Kuna miundo miwili ya vifungu vya maneno katika nyimbo za kampeni za Kichuka. Kwanza, kuna muundo unaozingatia sarufi. Pili, kuna muundo mpinduo. Muundo huu unakiuka ule upatanisho wa kisarufi. Hata hivyo, ujumbe unaowasilishwa hueleweka. Mistari ya vifungu vya maneno katika nyimbo hizi inaweza kuwa mistari kifu au mistari mishata.

Mfano wa mstari kifu:

*Kura ni cia Petkay.*

Mfano wa mstari mshata:

*Muthomi akuthii:*

*Baliamenti ii*

**Kumbuka:**

Ungekuwa mstari kifu kama angesema:

*Muthomi akuthii baliamenti ii*

Hata kama kuna ukiukaji mwingi wa kanuni za kisarufi katika miungano mingi ya maneno katika nyimbo hizi, kuna mshikamano ambao unajengwa na vijenzi vingi vya mshikamano. Maneno na vifungu vya maneno vinavyopatikana katika nyimbo hizi hushikamana na kujenga aina fulani ya mahusiano ya kisemantiki au kimaana inayofanya ujumbe katika wimbo fulani wa kampeni wa

Kichuka kueleweka. Katika nyimbo za kampeni za jamii ya Wachuka, mna ujumbe ambao umewalenga wapiga kura. Ujumbe huu unawasilishwa kwa mtindo fulani. Mtindo huchunguza jinsi ujumbe unawasilishwa kwa matumizi ya njia na mbinu tofauti. Kulingana na Hochman (1985), mtindo ni namna ya kufanya kitu kwa kufuata utaratibu fulani. Kwa uchaguzi wa mtindo katika nyimbo hizi, tunaona namna wanasiasa wanavyojitetea na kupinga kwa lengo la kuzipata kura. Kulingana na aina ya lugha wanayotumia ni wazi kuwa katika ngazi rafu ya malengo yao maishani, haja ya kupata nguvu za kisiasa ndiyo i juu kabisa. Ilivyo ni kuwa umilisi wa nguvu hizi huandamana na heshima, uwezo wa kiuchumi na pengine starehe fulani. Lugha inayotumika pale ni lugha teule ambayo inalenga kumdumisha au kumkweza kisiasa na wakati huo huo kumbomoa mpinzani. Malengo ya aina hii yatamfanya aweze kuwashutumu, kuwatukana na hata kuwakashifu wapinzani. Kwa ufupi wanasiasa wanatumia lugha ya kuwatisha wapinzani wao. Kwa mfano angalia vitisho vinavyopatikana katika wimbo ufuatao:

**Kichuka**

*Na Kareke:*

*Niarumithue mbumbui*

*Ya matina:*

*Agendage nayo.*

**Tafsiri**

Kareke:

Aumizwe buibui

Ya matako:

Kila wakati.

Nyimbo hizi za kampeni katika jamii ya Wachuka zimejaa propaganda na hata ukariri mwingi ili kuangazia uzuri au ubaya wa mwanasiasa. Kwa ufupi mitazamo ya wanasiasa inawafanya watumie lugha ya kusifu, kukashifu, kutia chumvi, kutusi na kuahidi. Kila wimbo wa kampeni katika jamii ya Wachuka ni usemi ulio na ushikamano fulani. Halliday na Hassan (1976) wanasema kuwa vijenzi vya mshikamano katika usemi husika huchangia kwa kiwango kikubwa udhahiri wa ujumbe unaowasilishwa. Dhana ya mshikamano katika muktadha huu inarejelea vijenzi vinavyofungamanisha au kushikamanisha wimbo fulani na kuufanya uonekane kuwa matini moja. Mawasiliano yoyote yale katika wimbo hutegemea kuwepo kwa mshikamano ili pawepo na mantiki, maana na uelewekaji wa kinachozungumziwa. Vijenzi mbalimbali vinaweza kutambuliwa katika kila wimbo lakini ufasiri wa ujumbe katika wimbo lengwa lazima utilie maanani uwepo wa pamoja wa vijenzi hivi. Vijenzi hivi ni pamoja na jina la wimbo, ujumbe, uwiano wa kisarufi, urejelezi, wahusika na kadhalika.

**Hitimisho**

Katika makala haya, tumeangalia mikakati inayotumiwa na wanasiasa katika jamii ya Wachuka ili kupata mamlaka na kujidumisha hapo kupitia nyimbo za kampeni. Tumefaulu kufanya hivi kwa kwanza kuangalia namna wanavyousawiri muktadha wa nyimbo hizi. Baada ya kuuangalia muktadha huo, tumeonyesha kuwa mchakato wa kisiasa katika eneo hili unazungukia wahusika fulani na hasa

wahusika wanasiasa halisi ambao wanazitaka nyadhifa hizo za kisiasa. Ni kupitia ujumbe unaobembeleza, unaokashifu na unaofahamisha wanasiasa hawa wanalenga kuyumbisha matamano ya wapiga kura ili waweze kuwapatia mamlaka ya kisiasa. Tumeonyesha kwamba wanasiasa katika jamii hii wamekuwa wakitumia lugha kwa namna inayowavutia wapiga kura wanaoishia kuwapatia mamlaka ya nguvu za kisiasa. Bourdieu (2001) anasema kuwa ni kupitia lugha wanasiasa huwanyang'anya watu wa kawaida mamlaka ya kisiasa na kujitwika wao. Wanasiasa wa Chuka wako radhi kutumia lugha kwa njia hasi au chanya, mradi tu waweze kuyumbisha akili za wapiga kura upande wao. Hili ni dhahirisho la namna lugha ilivyo muhimu katika maisha ya binadamu. Umilisi wa lugha na uwezo wa kuitumia kufuatilia malengo ya mwanasiasa ni chanzo cha nguvu na mamlaka ya kisiasa katika jamii hii. Ili pawe na mshikamano wa kitaifa na uwiano Barani Afrika, ipo haja ya wanalugha na wanafasihi kushirikiana na washikadau wengine kuhamasisha wapiga kura au umma kwa ujumla kuhakiki ujumbe na jinsi unavyowasilishwa kupitia nyimbo za kampeni ili kuweza kufanya maamuzi ya kisiasa yanayofaa. Kwa kuchanganua usemi wa nyimbo za kampeni za Wachuka, tumedhahirisha kuwa nyimbo zinaweza kutumika kwa njia hasi au chanya.

### Marejeleo

- Bourdieu, P. (2001). *Language and Symbols Power*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Fowler, R. na Wengine (1979). *Language and Control*. London: Routledge na Kegan Paul.
- Guthrie, M. (1967). *The Classification of the Bantu Languages*. London: International African Institute.
- Halliday, M. na Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. London: Longman Group.
- Hochman, B. (1985). *Character in Literature*. London: Cornell University Press.
- Madumulla, S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.
- Matei, A. K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mathooko, P. M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.
- Msanjila, Y. (1989). "Sociolinguistics – Rules of Formal Address in Kiswahili" katika *D.P.B. Massamba (Whr). Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Toleo 56*. Dar es Salaam: TUKI uk. 47-65.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mukuthuria, M. (1997). "Njeo katika Kitenzi cha Kitigania." *Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mwaniki, K. (1982). "Pre-Colonial History of the Chuka of Mt. Kenya." *Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa)*. Dalhousie University.

- Njogu, K. (2001). (Mhr). "Kimondo, Satire and Political Dialogue: Electioneering through Versification" *Research in African Literature*. Toleo 32 (1) = 1-13. Bloomington: Indian University Press.
- Nyairo, J. (2005). "Popular Music, Popular politics: Unbwogable and the idioms of Freedom in Kenyan popular Music. "Katika Jarida la *African Affairs*". Toleo 104 Oxford University Press.
- Senkoro, F. (1987). *Fasih na Jamii*. Dar es Salaam: Press & Publicity Centre.
- Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasih*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wa Mberia, K. (1993). "Kitharaka Segmental Morphophonology with Special Reference to the Noun and Verb." Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasih Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publication.
- Were, G. na Wilson, D. (1972). *East Africa through a Thousand Years*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.
- Wodak, R. (1995). *Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis*. Amsterdam: John Benjamins.
- Yule, G. (1985). *The Study of Language: an Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.